

Maswali

1. Kwa kitabu kipi katika Biblia tunasoma habari za Balaamu?
- 2.
3. Mfalme Balaki alitoka kwa taifa gani?
4. Mbona mfalme Balaki aliogopa Waisraeli?
5. Mbona Mungu alimwambia Balaamu asilaani Waisraeli?
6. Mbona Balaamu hakumtii Mungu?
7. Balaamu alimpiga punda wake mara ngapi?
8. Baraka gani za Waisraeli zilimuonekana Balaamu kwanza ?
9. Hizi baraka zitatimizwa lini kikamulivu?
10. Nani ndie kiongozi mkuu?

Majibu

1. Hesabu.
2. Ya arobaini.
3. Moabu
4. Alikuwa amesikia vile walishinda wafalme wengine ,tena walikuwa wengi.
5. Kwa sababu walikuwa wateule wa Mungu na wamebarikiwa?
6. Kwa sababu alikuwa mlafi
7. Mara 3.
8. Kwamba Israeli litakuwa taifa kubwa, na Mungu atawaongoza washinde. Tena kutakuwa na kiongozi mkuu atakayeshinda adui wao wote.
9. Wakati Ufalme wa Mungu utasimamishwa.
10. Bwana Yesu kristo

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



7 Hadithi ya Balaamu

Marejeo

Hesabu 22—24

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba hata tukijaribu kuzuia na kuharibu mipango ya Mungu, lazima ni mapenzi yake ndiyo yatatimizwa.

Maneno maalum

1. Waisraeli + Moabu + Balaki +ogopa
2. Balaamu + laana + fetha na dhahabu
3. Malaika + punda + piga
4. Uwezo wa kunena
5. Dhabihu + bariki + Mungu aliweka kwa mdomo wake
6. Taifa kubwa + shinda + Mfalme + Yesu + Ufalme wa Mungu.

7.1 Waisraeli walikuwa ni wamaana kwa Mungu, lakini walikuwa wameasi Mungu na Mungu akawazungusha jangwani kwa miaka 40 kama adhabu. Katika mwaka wa mwisho walipiga kambi kwa nchi tambarare ya Moabu. Balaki ndiye alikuwa mfalme wa Moabu wakati huo, na aliogopa kwa sababu alikuwa amesikia vile Waisraeli walikuwa wameshinda mfalme wa Amoni. Aliogopa kwamba yeye naye atakuwa hivyo.

7.2. Wamoabu hawakuamini Mungu wa Israeli. Badala yake mfalme Balaki aliamini ushirikina na madakitari wa uchawi. Alituma wajumbe kwa Balaamu aliyekuwa nabii wa uongo ili aje atabiri yatakayokuwepo kwa nchi yake. Alisema, “Kuna watu wengi sana kutoka Misri hata wamefunika nchi nzima. Kuja uwalaani kwa sababu wananishinda kwa nguvu. Niweze kuwashinda na niwafukuze watoke nchini.” Mfalme Balaki alinuia kutoa fedha na dhahabu nyingi na angepea Balaamu chochote alichotaka. Mungu alimwambia Balaamu ASIENDE kuwalaani kwa sababu Waisraeli ni watu wateule na wamebarikiwa. Balaamu alikubali malipo kutoka kwa mfalme Balaki kwa pupa.

7.3 Balaamu aliamka asubuhi ifwatayo, akaenda kwa punda kumuona mfalme Balaki. Lakini Mungu alimkasirikia Balaamu kwa sababu hakumtii. ,Akatuma malaika asimame njiani mbele yake ili amzuie. Punda alipoona malaika mbele yake ameshika upanga, alihepa kutoka njiani. Balaamu akawa na hasira na kumpiga kwa fimbo yake. Liendelea hivo mpaka mguu wa Balaamu ukakwarushwa kwa ukuta. Akampiga tena. Malaika aliwaelekeza kwa njia nyembamba penye punda hangeweza kugeuka kushoto wala kulia, kwa hivyo alilala chini.



Balaamu alikasirika tena na akampiga punda mara ya tatu kukataa kuenda .

7.4 Jambo lisilo la kawaida lilitendeke. Mungu alimwezesha punda kuzungumza. Soma Hesabu 22:28-30. Lazima Balaamu alishangaa lakini aliendelea kumpiga punda kwa hasira. Mungu alimwezesha Balaamu kumuona malaika. Malaika alimwambia Balaamu kwamba Mungu ame-udhika naye kwa kutomtii, lakini akienda kuona Balaki, amwambia mambo yenye Mungu amemwekea mdomoni.

7.5 Mwishowe Balaamu alifika kwa jumba la mfalme Balaki na wakakwea kilima ili waone kambi ya Israeli ndio Balaamu awalaani. Walitoa dhadihu nyingi halafu Balaamu akaanza ...LAKINI, Mungu alitumia Balaamu kubariki Waisraeli. Alijaribu mara tatu kulaani lakini kila wakati alisema maneno yaliyowekewa mdomoni na Mungu. Kawaida hii ilimkasirisha mfalme Balaki. Alitaka Balaamu alaani lakini Mungu hangeruhusu watu wake walaaniwe. Kama adhabu, Mungu akaendelea kusema kupitia kwa Balaamu kwamba Moabu itaadhibiwa na Waisraeli.

7.6 Alipokuwa akibariki Balaamu alitabiri kwamba Israeli litakuwa taifa kubwa na Mungu atawaongoza Waisraeli washinde. Tena alizungumzia juu ya kiongozi mkuu mwenye wakati ujao atakuwa mfalme na awaongoze kushida adui wao. Kwa sehemu utabiri huu ulitimizwa wakati Yohana aliwaongoza Waisraeli katika nchi ya Ahadi na baadaye Mfalme Daudi akayashambulia na kushinda mataifa yaliyokuwa karibu. Walakini haya yote yatatimizwa wakati Bwana Yesu Kristo atakaporudi hapa duniani kama Mfalme wa Wayahudi kusimamisha Ufalme wa Mungu.